



GRETSIA UNIVERSITY - THIKA

UNIVERSITY EXAMINATIONS MAY-AGOSTI 2023 SEMESTER

BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

KODI: KISW 402

KOZI: UHAKIKI WA FASIHI YA KISWAHILI

TAREHE: 2 AUGUST 2023

WAKATI: 3:00 PM – 6:00 PM

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MATATU**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTIHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. **ANDIKA VIDOTEKO VYAKO NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU KISHA**
PIGIA MSTARI BAADAYE

TAHADHARI:-kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani

SEHEMU YA A: YA LAZIMA

SWALI LA KWANZA

- a) Huku ukitaja mifano, vijadili vipengele vine vya uhakiki wa fasihi. [Alama 12]
- b) Kwa kutaja mifano, fafanua umuhimu wa mbinu zifuatazo za Sanaa katika kazi za kifasihi:
 - i. Taswira [Alama 2]
 - ii. Sadfa [Alama 2]
 - iii. Ndoto [Alama 2]
 - iv. Barua [Alama 2]
 - v. Wimbo [Alama 2]
- c) Yaeleze masuala manne muhimu ambayo huangaziwa wakati wa kuhakiki tamthilia. [Alama 8]
- d) Dhihirisha jinsi wahusika wowote wawili wanavyochangia katika ukuzaji wa maudhui katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* ya K.W. Wamitila. [Alama 8]
- e) Taja aina zozote mbili za uhakiki wa fasihi. [Alama 2]

SEHEMU YA B: YAJIBU MASWALI YOYOTE MATATU

SWALI LA PILI

- a) Fafanua masuala manne yanayoangaziwa katika riwaya ya *Siku Njema* ya Ken Walibora. [Alama 12]
- b) Wanawake katika jamii ya sasa ni wanamapinduzi. Jadili huku ukirejelea tamthilia ya *Kilio cha Haki* cha A. Mazrui. [Alama 08]

SWALI LA TATU

- a) Bainisha namna ambavyo Ken Walibora ametumia motifi ya safari kuendeleza hadithi iliyomo katika riwaya ya *Siku Njema*. [Alama 4]
- b) Yaeleze mapungufu yoyote matatu ya usimulizi katika nafsi ya kwanza. [Alama 6]
- c) Waandishi wa riwaya za Kiswahili huwatumia wahusika vijana kuleta mabadiliko katika jamii. Jadili huku ukitaja mifano. [Alama 10]

SWALI LA NNE

- a) Yatalii maudhui yoyote manne yanayojitokeza katika mashairi yaliyomo katika diwani ya *Msimu wa Tisa* ya Kithaka wa Mberia. [Alama 12]
- b) Huku ukidhihirisha mifano, fafanua mbinu zozote nne za lugha ambazo Kithaka wa Mberia amezitumia katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. [Alama 08]

SWALI LA TANO

- a) Waandishi wa kazi za fasihi huandika kutokana na tajriba zao. Fafanua huku ukitaja mifano kutoka kazi za Kiswahili. [Alama 10]
- b) Huku ukitaja mifano kutoka kazi za Kiswahili, zieleze dhana zifuatazo:
 - i. Uchimuzi [Alama 2]
 - ii. Msuko [Alama 3]
 - iii. Dhamira [Alama 2]
 - iv. Usimulizi [Alama 2]